WANJIGI APONGEZA MATAIFA YA AFRIKA KWA UMOJA WA KUKABILI MATITIZO YA ELIMU

na
S. A. AL-ISMAILLY

NAIBU Waziri wa Elimu Bwana Maina Wanjigi wiki hii amewakaribisha wajumbe wanaohudhuria mkutano wa Wanachama wa kamati kuu ya Muungano wa Lattabs za mafunzo ya Sayansi katika bara la Afrika aliouzungua rasmi mjini Mombasa katika Chuo cha Mombasa Polytechnic mnamo tarehe January 15 mwaka huu.

[illegible]

kuwa juhudi za pamoja kumaliza matatizo ya [illegible].

Alisema "Kwa wakati huu Umoja huu umeshughulisha [illegible] wa walimu wa [illegible] katika shule za msingi [illegible] mafunzo ya walimu juhudi za kushirikiana katika mipango ya elimu."

Alisema umoja huo wa SEPA umekuwa ukishirikiana na nchi za mipango ya mafunzo katika Mataifa ya Ethiopia, Gambia, Ghana, Kenya, Lesotho, Malawi, Nigeria, Sierra Leone, Tanzania, Uganda na Zambia." Alisema umoja huo umeanzisha mpango kadha wa kadha yenye lengo la kuwasaidia [illegible] na ndani ya shule kufaidika.

Mkutano huo unahudhuriwa na wawakilishi kutoka Kenya, Nigeria, Ghana, Lesotho, Tanzania, Liberia. Makao makuu ya Umoja huo yapo huko mjini Accra nchini Ghana.

KATIBU Mkuu katika wizara ya utalii akipokea nakala ya Wasifu wa Moi kutoka kwa Mhariri Faraj Dumila. Anayefuata ni Bwana Chege, Mkuu wa kuchapisha vitabu katika Idara ya Kenya Literature Bureau.

Wasifu wa Moi
Mhariri: Faraj Dumila
Mungo Chege, Kenya Literature Bureau
Bei: Sh [illegible]

WASIFU WA MOI ni mkusanyo wa mashairi yenye kueleza maisha ya Mtukufu Rais Moi, uwongozi wake na vile alivyotabiki kuonzli Urais wa Serikali ya Jamhuri ya Kenya na Chama Kinachoongoza Serikali, Kanu.

Mashairi mengi yametoka katika mjas wa Pwani yakiwa kule kuwasili kwake huko Pwani kwa mara ya kwanza na kupokewa kwa shangwe kuu.

Miongoni mwa washairi wa Pwani walioshiriki katika uandikaji wa kitabu hiki ni pale lingwa mashuhuri Sheikh Ahmed Nabahani, Maalim Mohammed Kamal Khan, Zainab Haji, Sudiye Mohammed Mhandisi, Issa M. Issa na Bobby.

Mashairi yao yameeleza kwamba mapenzi na upendo walio nao wananchi wanayo kwa kiongozi wao mpya Mtukufu Rais Moi.

Kwa kweli hiki ni kitabu ambacho katika kila shule kuweko na kiti ningi ambazo zitasomwa na wanafunzi ambao wengependa kuona vile wananchi wanavyotaa kutopenda kiongozi wao.

Sina shaka walimu wanafunza somo hili katika shule zetu za kigeni watakichungua kitabu hiki kwa makini na kushauri halmashauri mayo Jamika na kukubali vitabu visomwe kama kazi ya mtihani.

Wasifu wa Moi kwa jumla ni kitabu kitachowawezesha wanafunzi wa vidato totauti kukitumia kwa kuimba nyimbo yenye kuonyesha mapenzi kwa kiongozi Rais Moi, wananchi na Taifa la Kenya.

KWA UFUPI

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake, Mombasa, Bi Dina Mshenga amewapongeza wanawake wa Mombasa kwa umoja wao uliorahisisha ujenzi wa makao yao makuu huko majengo kwa gharama ya shilingi 250 elfu. Ujenzi huo unatarajiwa kumalizika mwisho wa mwezi wa March mwaka huu.

AFISA MKUU wa Mipango ya maendeleo Pwani, Bwana A. A. Mwinamo amesema mpango wa makao wa Magarini huko wilayani Kilifi utatoa nafasi jaz kwa zaidi ya jamii elfu 4.

MWENYEKITI wa baraza la mji wa Malindi Diwani Mzee wa baya ametoa mwito kwa wananchi kutoa maombi kwa mpango wa makao mapya huko Malindi.

HUKO Lamu, Mwanachama wa halmashauri ya Elimu, Bwana H. Saleh amepongeza hatua ya afisa Mkuu wa Elimu wa Lamu kwa kuidhinisha kutoa mafunzo ya Dini katika shule za serikali hatua ambayo itawatia moyo wazazi kuwapeleka watoto wao shuleni.

GLADYS OSORO

na
PETER KILEMBA

Binti Gladys Osoro ni mmoja wapo wa wasichana waliyojiunga na Umoja wa 'Association for Education and Development' nchini Kenya na alipohojiwa alisema "Nilijiunga na umoja huo ili kurekebisha matatizo yanayokabili jamii, na hasa kuona kwamba hatua za kushirikiana za kujenga Kenya moja tuipendayo."

Binti Osoro alizidi kusema "Umoja huo uliniwezesha kushirikiana kindugu na wananchi wenzangu wa Kenya kutoka sehemu zote za taifa hili na hata kupata nafasi ya kushirikiana na wenzetu kutoka mataifa ya mbali kama vile Japan na kadhalika."

Aliendelea "Umoja wa AED unajenga jamii bora ya ushirikiano upendo na maendeleo valiyo na msingi wa amani, na kwamba vijana wanapata mafunzo ya kuwa raia wema wenye kujua dhamani zao kwa taifa lao na watu wao."

[illegible]

NJE YA SHULE

Waziri alisema "Tatizo kubwa [illegible] wanafunzi wengi watu [illegible] wapata 73 kwa 100 [illegible]."

[illegible]

MWENYEKITI

Mwenyekiti wa Halmashauri [illegible] Bwana Ephantus M. Mugo wa Chuo cha Mafunzo ya Elimu cha Kenya, alisema Mkutano huo una lengo la kuongoza juhudi za mafunzo kwa njia wahusika nje ya shule.

Alisema tangu kuanzishwa umoja huo wa Kiongoza mafunzo katika bara la Afrika huko Sierra Leone mwaka 1970 umoja huo umeleta mengi. Alisema lengo la kwanza hili [illegible]

TUFUATE NJEMA NYAYO

Mhariri tafadhali,
Fanya ala kuli hali,
Lichapwe shairi hili,
Shime wa Kenya soteni,

Yo sawa ayasemayo,
Tuyafuate kwa moyo,
Hima tuandame nyayo,
Shime wa Kenya soteni,

Tuache tikira mbovu,
Ni sumu inlaya uvivu,
Shime umoja ni nguvu,
Shime wa Kenya soteni,

Nakuomba kwa hisani,
Ijapokuwa pembeni,
Utokeze gazetini,
Tufuate njema nyayo.

Raisi wetu jamani,
Neema ye nchini,
Tufikie kileleni,
Tufuate njema nyayo.

Twaitia hatarini,
Wa Kenya tahadharini,
Upweke ni kitu duni,
Tufuate njema nyayo.

Ni zako Moi pongezi,
Wewe mbye kiongozi,
Uiongoze tahazi,
Shime wa Kenya soteni.

Kadhamati shairi,
Rabi mpe Moi heri,
Uzuri wake umuri,
Shime wa Kenya soteni.

Unjali aslani,
Ukamate usukani,
Ifikie bandarini,
Tufuate njema nyayo.

Yatosha nilobaini,
Ili awe furahani,
Na kuishi kwa amani,
Tufuate njema nyayo.

ALI SALIM MUHSIN
MOMBASA.

Coastweek *** JEMBE

JEMBE
UNGA SAFI
WA MAHINDI

SWAHILI CROSSWORD NO. 10



JINA......................................

SANDUKU LA POSTA.......................

....

KWENDA KULIA:
1. Janbio
6. Neno la kushtuka
7. Aina ya mmea uzaao matunda
9. Koo
11. Kimempotea, kimemghibu
12. Posuka, pea
15. Ukambaa mwembamba
17. Mfanti wa mashua
18. Ubongoni

KWENDA CHINI:
2. Codoro
3. Heko, pongezi
4. Kupata salam, kuokoka
5. Vunja
8. Jina jingine la Salimu
10. Kupanga miti juu ya dari
12. Ni moto kisha ni mnyama wa baharini
13. Sehemu ya mmea
14. Ghiya, juhudi
15. Wa kufukuzia
16. Itoe roho

Washindi wa Fumbo La Kujaza Maneno No. 8:
[1] Anne Wambui c/o Jecinta, Sanduku la Posta 90181 Mva
[2] Esther Mwabili, c/o S. Mwabili Jeremy, Sanduku la Posta 90181, Mombasa
Washindi wanombwa wafike Afisini mwa COASTWEEK

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 8

KWENDA KULIA:
1. UO 3. KU 4. DAA 7. SUDI 9. PONO 10. UMUA 11. UGUA 12. BANIKA 17. WAMBO! 20. ANIA 22. AUNI 23. TANA 24. KUTU 25. AOA 26. NI 27. OI

KWENDA CHINI:
1. USURU 2. OUMA 3. KYM 4. DOG 5. ANUA 6. AUA 8. DUNI 9. PUA 13. KWA 14. ABUU 15. AIUI 16. ANAO 17. WAA 18. MAKI 19. ONYO 20. ATA 21. INA

Shindano la fumbo la kujaza maneno.

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayosikilizwa.

Washindi wawili wa kwanza kila mmoja atapatiwa baridali moja la Unga Wa Mahindi chapa Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK LTD. pamoja na ATTA LTD. Mombasa.

Jawabu za fumbo hili zipelekwe kwa mhariri COASTWEEK, sanduku la posta 87270, Mombasa, Kenya, siku ya Alhamisi tarehe 25.1.79, siyo sita mshiriki shindano hili [illegible].

POSITIVELY BEST BARGAINS OF THE WEEK
Coastweek T-SHIRTS
ONLY 26/= EACH FROM COASTWEEK MOMBASA OFFICE